JINA_____ **KIDATO**_____

TAREHE _____ **SAHIHI** _____

102/2
KISWAHILI LUGHA
KIDATO CHA NNE
MUHULA WA KWANZA 2016
SAA 2½

Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari Nchini Kenya
KISWAHILI PP 102/2
KIDATO CHA NNE MUHULA WA KWANZA 2016

Maagizo:

- Jibu maswali **yote**

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

	Swali	**Upeo**	**Alama**
1.	**Ufahamu**	**15**	
2.	**Muhtasari**	**15**	
3.	**Matumizi ya lugha**	**40**	
4.	**Isimu Jamii**	**10**	
Jumla		**80**	

Mtahiniwa ahakikishe kwamba karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa

Sehemu I: Ufahamu (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:

Nyumba ya Ndolo ya vyumba viwili ilikumbwa na hali mbili tofauti usiku huo. Chumbani alimolala Ndolo mwenyewe, kimya cha kaburi kilikatizwa na misono yake. Mara mojamoja alijigeuza kitandani na kuzifanya mbavu za kitanda zilalamikie uzito wake. Katika chumba kingine, misono ya Ndolo na milio ya chenene ilimkirihi Msela. Kuzidisha, mawazo kuhusu hali ya mamake na unyama aliotendewa babake yalimtoroshea usingizi. Akasalia kujilaza kwenye mkeka wake.

Kila alipotafakari maneno ya mzee Ndolo ndivyo Msela alivyozidi kuamini kwamba matatizo ya familia yao yalisababishwa na Mzee Bonga. Lakini yote hayo akayapuuza. Kubwa kwake lilikuwa ni kumwona mama yake na kujua ni hatua gani atakayochukua licha ya uzito aliouona mbele yake kwa kutokuwa na kipato. Msela alijikuta kwenye mtihani mgumu ulioifanya mishipa ya kichwa kusimama na kichwa kumuuma.

Kwa sababu ya maumivu hayo, msela alijisogeza na kujiegemeza kwenye ukuta. Akawa anatazama jinsi Mungu alikuwa akiufanya muujiza wake ambao alikuwa ameukosa kwa muda. Alifurahi kuliona jua likipenyeza miale yake kisha kujitokeza na kuangaza dunia. Ingawa macho yake yalifurahia mapambazuko hayo, moyo wake ulikuwa na machungu. Akili yake ilikuwa na zigo zito la kutafuta ufumbuzi ambao kwa upande wake ulikuwa ni ndoto.Msela alijiuliza mengi katika nafsi yake. Aliisaili nafsi yake kuhusu hisi za ndugu zake, kuhusu hali ya mama yao aliyesemekana kuwa mwendawazimu, na ikiwa walifahamu hilo. Alitaka kujua alikokula na alikolala mamake katika hali yake hiyo. Kila f ikira iliyompitikia akilini ilitaka kupasua mishipa ya kichwa chake. "Ina maana hawaoni au nao wamekuwa na roho ya korosho kama Mzee Bonga?" Alijisaili Msela. Katika maswali yote hayo, alikosa majibu isipokuwa kuzidisha maumivu ya kichwa. Isingekuwa kwa machozi yaliyompunguzia baadhi ya machungu, labda angegeuka hayawani.

Macho ya Msela yalikuwa yamevimba, tena mekundu kutokana na ukosefu wa usingizi. Mwili wake nao ulionekana kunyong'onyea kwa sababu ya mazonge ya mawazo. Alichukua kikopo kilichochoka cha maji na kunawa uso kisha akaenda kukaa juu ya jiwe. Kibaridi kilichotokana na mvua iliyokuwa ikinyesha kilimpiga lakini hakujali. Angejali vipi yeye katika mtafaruku wa mamake?

Ingawa Mzee Ndolo alimwita ndani ili aipishe mvua, Msela alidinda. Badala yake, aliendelea kuuachilia mwili wake kuloweshwa na michonyoto ya mvua. Kila alivyofikiria maisha ya mwendawazimu ndivyo moyo ulivyozidi kumuuma. Akawa yuajiuliza mama yake aliukosea nini ulimwengu hata apate adhabu ile. Halafu fumo lake la mwisho moyoni ni madhara ya mvua na baridi ile kwa mamake. Hana makao, hana mavazi mazito, hana chochote! Alipowazia makazi ya jalalani na majumba mabovu ambayo siku zote amekuwa akiwaona wendawazimu wakifaliwa kwayo, aliachama.

Maswali:

a) Eleza ukinzani ulio katika nyumba ya Ndolo. (alama 2)

b) Ni yapi yaliyomkosesha usingizi Msela? (alama 3)

c) Kwa nini Msela hakuweza kuibadili hali yake? (alama 4)

d) Taja chanzo cha madhila ya Msela. (alama 1)

e) Muujiza wa Mungu unatoa taashira gani kwa hali ya msimulizi? (alama 2)

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

i) Roho ya korosho

ii) Kunyong'onyea

iii) Aliachama.

Sehemu II: Ufupisho (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo:

Tunafurahi sana tukiangalia vile Kiswahili kilivyopiga hatua lakini watu wajue kuwa ukiviona vilivyoelea vimeundwa. Kiswahili kimetoka mbali na kimefanya watu wengi watoe jasho katika kukikuza. Kiswahili kimekuwa na vikwazo vya hapa na pale kilipo leo. Hawajachoka kukiza na kukieneza.

Hapo awali watu wengi walipendelea lugha zao kuliko Kiswahili kwa hivyo nafasi ya Kiswahili ilipenya kwa ugumu hasa katika makabila ya bara. Watu wengi waliokipenda Kiswahili walichukuliwa kama waswahili laghai. Waswahili wenyewe nao waliwaona watoka bara kama washamba na basi ikawa ni kikwazo cha kutoendelea kwa Kiswahili kwa urahisi katika sehemu za bara.

Wakati huo pia njia za mawasiliano zilikuwa si nyingi. Hali ya kijiografia nayo haikuruhusu kwani sehemu za mwambao zilitengwa na zile za bara kwa misitu na mbuga zilizokuwa na wanyama wakali. Watu waliogopa usafiri kwani hata hapakuwa na magari. Kiswahili pia kilikuwa ni kigumu kwa watu ambao asili ya makabila yao si ya kibantu. Kwao ngeli za Kiswahili ziliwapatia shida na kwa hivyo walichukua muda kukijua.Kihistoria pia tunaambiwa kuwa sehemu za Kenya na Uganda hazikuingiliwa sana na waarabu na pia misafara ya watumwa iliyokuwa ina watu waliojua Kiswahili haikuwa mingi kama vile ilivyokuwa nchini Tanzania. Kwa hivyo ilichukua muda kwa watu wa bara katika nchi hizi kukijua Kiswahili kwani hawakuwa wakikutana mara kwa mara na hawa watoka pwani.

Wakoloni walipokuja, wengine hasa Wajerumani walihimiza kutumiwa kwa Kiswahili lakini kwa wale watoka bara waliokuwa wanauchukia utawala wa Wajerumani hawakuona haja hata ya kujikaza kujua Kiswahili.

Wapo baadhi ya wakoloni ambao walipinga kuendelea kwa Kiswahili kwani walisema Kiswahili ni Kiislamu. Wakristo wengi wa awali walifunzwa dini kwa lugha zao za kimama na hili ni jambo lililozorotesha Kiswahili.

Baadhi ya Waafrika hawakuwa wamesoma, kwa hivyo Kiswahili chao kilikuwa kile cha kuokotezaokoteza mitaani; Kiswahili cha kuombea maji tu.Baadhi ya watawala katika miaka ya thelathini walianza kuogopa nguvu za Kiswahili wakataka wakomeshe matumizi ya Kiswahili mashuleni ili kisije kikawaunganisha Waafrika. Hapo walikuwa wameambulia nunge kwa kuwa Kiswahili kilikuwa kinakua kwa haraka licha ya pingamizi zote hizo.

Wasomi wachache waliathiriwa sana na Kiingereza. Badala ya kukikuza Kiswahili walikuza lugha za kigeni na kuona Kiswahili kuwa lugha duni, wakihisi hawatatambulika kama wasomi. Kasumba hii ilirudisha Kiswahili nyuma kiasi kwamba iligeuka kuwa kicheko kwani wataalamu wa Kiswahili walioisanifisha lugha, wengi walikuwa ni wazungu Waafrika waliojua lugha vilivyo pamoja na utamaduni wake walijitoa katika utaalamu na katika maamuzi yaliyohusu kukua na kuenea kwa Kiswahili. Walisahau kabisa kuwa huo ulikuwa ni wajibu wao.

Ingawa Kiswahili kiliwaunganisha watu wengi hadi walipopata uhuru, nchi nyingi hazikukitumia kama lugha ya taifa mara moja. Kiswahili hakikuwa somo la lazima isipokuwa nchini Tanzania. Kiswahili kilidharauliwa na walimu walikuwa haba sana na hata wanafunzi wa somo hili walikuwa wachache.

Athari za lugha za kimama na za kigeni, kwa kiasi fulani zimefany watu wasijiamini katika lugha ya Kiswahili. Vijana wa sasa nao wanazidi kuiharibu lugha kwa kutumia "Sheng"! Jambo ambalo pia linaudhi na linalorudisha maendeleo ya lugha hii nyuma ni kuwa, watu wengine hujiingiza katika shughuli nyingi za lugha hii, si kwa sababu wanaipenda au wanaijua; la, ila wanataka tu wajipatie unga.

Isitoshe muungano kamili wa wasomi wa Kiswahili bado haujapatikana sawasawa. Badala ya kusaidiana, kuna dharau, ndaro za ajabu na pia mashindano mengi ya kitoto. Badala ya kuongozana, wivu, dharau, uwongo na fitina vimetawala baadhi ya watu. Taabu zote hizi zitakapopungua au kuisha kabisa, ndipo Kiswahili kitakapozidi kukua na kupendwa.

Maswali:

a) Kwa kutumia maneno 100, fafanua pingamizi zilizokuwepo hapo awali kabla ya uhuru kuhusu kukua kwa Kiswahili (alama 9)

Matayarisho

Jibu

b) Kufikia sasa kukua kwa Kiswahili bado kunakabiliwa na matatizo mengi. Yaeleze matatizo haya kwa maneno 55-60 (alama 6)

Matayarisho

Jibu

Sehemu III: Matumizi ya Lugha (alama 40)

a) Tambua aina za mofimu zilizopigiwa mstari (alama 2)
Saa *sita* ilipofika *alisita* na kumuaga mgeni wake.

b) Andika maneno yafuatayo katika kauli zilizo mabanoni (alama 2)

i) Unga (tendama)

ii) Sokoa (tendata)

c) Eleza matumizi ya kiambishi 'ji' na 'ku' katika sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Jibwa lilibweka usiku kucha

_____

ii) Kucheza kwake kunaridhisha

_____

d) Geuza kwa ukubwa (alama 3)
Mzee yule alikalia ngoma ile kama kiti

_____

_____

e) Unda vivumishi kutokana na vitenzi hivi (alama 2)

i) Kakamaa

_____

ii) Samehe

_____

f) Sahihisha (alama 2)
Kitabu yake ilitupwa katika pipani

_____

_____

g) Andika upya bila kutumia 'amba' (alama 2)
Mtu ambaye atashinda ataapishwa.

_____

_____

h) Unda nomino za dhahania kutokana na vivumishi vifuatavyo (alama 3)

i) Bora

_____

ii) Safi

_____

iii) –chache

_____

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo jedwali (alama 4)
Wote walifikishwa mahakamani lakini walikanusha mashtaka.

j) Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo (alama 3)

i) Karonei ni mwanariadha hodari.

_____

_____

ii) Wachezaji wameingia uwanjani.

_____

_____

iii) Nileteeni chupa zile.

_____

_____

k) Tumia vielezi viwili vya mahali vya viambishi katika sentensi (alama 2)

_____

_____

l) Taja konsonanti mbili zinazotamkwa baina ya meno na mdomo. (alama 2)

_____

_____

m) Bainisha kirai katika sentensi ifuatayo na ueleze ni cha aina gani (alama 2)
Nyumba nyingine mpya imejengwa.

_____

_____

n) Kanusha (alama 2)
Mwajiri wao amekuja kuwalipa mshahara.

_____

_____

o) Akifisha (alama 3)
Ahh huu ndio ushauri aliotuitia mmoja wao aliropoka

_____

_____

p) Onyesha mzizi wa kila kitenzi ulichopewa (alama 2)

i) Hawajala

_____

_____

ii) Walipigania

_____

_____

q) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Aliyempeleka mjini alimtelekeza huko.

Sehemu IV: Isimujamii (alama10)
Huku ukitoa mifano, fafanua sifa zozote 5 za lugha inayotumiwa mkahawani (alama 10)